**OFISI YA RAIS UTUMISHI, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA UTAWALA BORA**

SHULE YA SEKONDARI MABWEREBWERE,
S.L.P 50,
KILOSA.
MOB: 0784275558 / 0713275558.
Tarehe: ............/............./.................

KUMB. NA. ...........................................................
JINA LA MWANAFUNZI ............................................................................
S.L.P ...........................................................................

**YAH: MAELEKEZO/MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MABWEREBWERE KIDATO CHA .................... MWAKA ....................**

## 1.0 Utangulizi

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechanguliwa kujiunga kidato cha ............. katika shule hii mwaka ...................... . Shule ya sekondari Mabwerebwere ipo umbali wa kilometa 12 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.
Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ........./......./.............. . Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ........../........./........... na mwisho wa kuripoti ni tarehe ........./......./............

## 2.0 Mambo ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

a) Sare ya shule hii ni:-
- **Wavulana:** Suruali mbili (2) pana na shati mbili (2) nyeupe za tetron mikono mifupi aina ya tomato, sox nyeusi na viatu vya ngozi vyeusi.
- **Wasichana:** Sketi mbili (2) ndefu na shati mbili (2) nyeupe za tetron mikono mifupi aina ya tomato, sox nyeupe na viatu vya ngozi vyeusi. Mshono wa sketi ni linda box. ***NB: Kitambaa cha rangi ya sketi na suruali kimeambatanishwa***
  - *Rangi ya hijjab kwa wasichana ifanane na sare ya shule*

b) Sare za michezo
- **Wavulana :** Bukta na tshirt zenye rangi ya blue
- **Wasichana:** tracksuit na tshirt za rangi ya blue

2.2 Daftari/counter books kumi (10), daftari kubwa za kawaida (msomi) kumi (10) kwaajili ya mazoezi, kalamu za wino za kutosha, penseli, rula na mkebe wa mahesabu (Mathematical Set).

2.3 Vitabu vya tafsiri ya lugha (dictionaries) mbili: Moja ya Kiingereza – Kiswahili na Nyingine ya Kiswahili – Kiingereza. **(English – Swalili Dictionary na Swahili – English Dictionary)**

2.4 Chakula cha mchana, matibabu na vifaa vya usafi kwa wasichana ni gharama ya mzazi.

2.5 Nauli ya mwanafunzi wa bweni kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro pamoja na vifaa vya malazi ni gharama ya mzazi/mlezi

**MUHIMU:**
***Mwanafunzi anapokuja kuripoti shuleni ni lazima awe amevaa sare ya shule iliyokamilika (full school uniform), pia aje na vifaa na mahitaji yote ya shule kama iliyoelekezwa. Mwanafunzi atakaekuja kuripoti shuleni akiwa kavaa nguo za nyumbani au hana mahitaji yalioelekezwa hatosajiliwa/hatopokelewa.***

## 3.0 Sheria na kanuni za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na na Mafunzo ya Ufundi; yenye dhamana ya Elimu chini ya Ofisi ya Rais Utumishi, Tamisemi na Utawala bora yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu nchini.
Unatakiwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na mambo mengine ya msingi utakayoelekezwa ukiwa shuleni. Zifuatazo ndio Sheria za shule

### 3.1 Sheria za jumla

Uvunjaji wa sheria zifuatazo utapelekea mwanafunzi kupewa adhabu kali na marudio yake yatasababisha mwanafunzi kusimamishwa masomo:

i. Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi/walezi, wafanyakazi wasiowalimu na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima. Ni lazima mwanafunzi asimame anapopita mwalimu, mzazi nk, na asalimie kisha apokee vifaa alivyonavyo. Vilevile wanafunzi wanatakiwa kuheshimiana na kushirikiana.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

iii. Kushiriki kwa umakini katika kufanya maandalio ya jioni (preparation). Ni lazima kila mwanafunzi awe na ratiba ya kujisomea nyumbani.

iv. Kuwahi katika shughuli za shule na kazi nyingine utakazopewa ni jambo la lazima.

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii. Ukitoka nje ya mipaka ya shule ni lazima uwe na kibali.

vi. Kutunza usafi wa mwili, malazi na mazingira ya shule ni lazima kwa kila mwanafunzi. Hii ni pamoja na kuokota uchafu ulio karibu yake.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote na ni lazima shati/tshirt ichomekwe kwenye sketi/suruali. Ni marufuku kuvaa viatu vya wazi (ndala/malapa/sendo) shuleni.

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

ix. Kutunza mali za Umma. Mwanafunzi atalazimika kufidia mali yoyote atakayoharibu au kupoteza.

x. Wanafunzi ni lazima waheshimu ofisi ya Mkuu wa Shule, ofisi za Idara, ofisi ya walimu, ukumbi wa chakula, maabara, maktaba na madarasa.

xi. Kuhudhuria masomo kwa wakati, kuandika nukuu za masomo, kufanya mazoezi, majaribio na mitihaniyote inayomhusu nakama kuna sababu ya kutohudhuria darasani au kutofanya zoezi, jaribio aumtihani ielezwe mapema.

xii. Kutii kengele kama mwito wa haraka. Mwanafunzi ni lazima akimbie kuelekea eneo la mkusanyiko au eneo husika mara tu asikiapo kengele.

### 3.2 Sheria za madarasani

Ukiukwaji wa sheria hizi utasababisha mwanafunzi kupewa adhabu kali

a. Keleze za aina yoyote haziruhusiwi darasani. Kumbuka darasani ni mahali pa kujifunzia, sio pa kupiga kelele.

b. Ni lazima kila mwanafunzi akae darasani kwakufuata mpango uliowekwa, kutofanya hivyo ni kukiuka sheria.

c. Hakuna mwanafunzi anaeruhusiwa kuandika ubaoni bila ruhusa ya mwalimu.

d. Hakuna mwanafunzi atakayetoka nje ya darasa wakati wa vipindi bila ruhusa ya kiongozi wa darasa.

e. Kuingia na chakula/kinywaji darasani au kula darasani.

### 3.3 Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi afukuzwe shule

i. Wizi wa aina yoyote, hata wa kuiba kalamu au daftari

ii. Uasherati, ubakaji, usagaji na ushoga

iii. Uvutaji wa sigara, bangi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya

iv. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu yeyote iwe shuleni au nyumbani

v. Kuoa au kuolewa

vi. Kupata mimba, kusababisha mimba, kutoa mimba au kusaidia utoaji wa mimba.

vii. Makosa ya jinai. Mfano kumtishia mwenzako kwa kumwambia **"UTAONA!"**

viii. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma

ix. Kughushi nyaraka za shule kama mhuri, saini ya mwalimu nk

x. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa au Fedha ya Taifa

xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

xii. Kukataa adhabu kwa makusudi bila kujali nani ametoa adhabu hiyo, mwalimu au kiranja.

xiii. Kupigana na mwanafunzi mwenzako, mwalimu, mtumishi asiyekuwa mwalimu n.k

xiv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro

xv. Kutoa lugha chafu/kejeli/matusi kwa mwanafunzi mwenzako, mwalimu, mzazi/mlezi au mtumishi asiyekuwa mwalimu ndani au nje ya shule.

xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni. Hii ni pamoja na kuuza pombe au bangi mahali popote pole ilimradi uonekane.

**3.4 Ni marufuku kufanya yafuatayo:-**

i. Kusuka nywele, kufuga nywele ndefu, kufuga ndevu, kunyoa upara au minyoo ya kihuni/isiyokubalika. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote

ii. Kupaka rangi za nywele, kupaka wanja, kupaka rangi za midomo au kubandika meno ya bandia.

iii. Kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha au kubandika kucha za bandia.

iv. Kujichora michoro/tattoo au maua mwilini

v. Kuvaa shanga, mkufu, heleni, bangili, pete, kacha, rozari au tasbihi

vi. Kujiremba, kutumia vipodozi vinavyobadilisha rangi ya ngozi au ***angel face***

vii. Kuvaa kanga, gauni, dila, sketi au suruali za kubana/jeans, fulana/blauzi za mabega wazi wakati wa masomo ya ziada/maandalizi hasa jioni au siku za wikiendi. Wakati wa masomo ya ziada ni lazima mwanafunzi avae suruali/sketi na T – shirt ya shule.

*MUHIMU*

***Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na nadhifu muda wote awapo shuleni, avae sare ya shule inavyostahili na ni marufuku kuvaa mlegezo/mlegesho.***

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi shuleni**

a. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule utakaporipoti shule

b. Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi /mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Fomu hii nayo utaikabidhi ofisini kwa Mkuu wa Shule

c. Fomu ya Mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maekekezo mengine yatakayotolewa na Uongozi wa Shule.

**5.0 Tafadhali soma kwa umakini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

Karibu sana Mabwerebwere Sekondari

"Elimu ni Hazina"

..........................................

IDRISA K. SELEMANI
MKUU WA SHULE

KIAMBATANISHO A: FOMU YA KUMUANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI
OFISI YA RAIS UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWALA BORA

SHULE YA SEKONDARI MABWEREBWERE

(jaza fomu hii kwa uangalifu)

| Picha ya mwanafunzi |
|---|
| |

1. Jina kamili la mwanafunzi...........................................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa......../......../.............Wilaya...................................... Mkoa.....................................

3. Kabila.......................... .......................Uraia.............................. ...........Dini....................................

4. Jina la mzazi....................................................................................................................................

Anuani ya Mzazi.................................................................................................................

Kazi ya Mzazi.........................................................................Simu na. ...................................................

---

**(Sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao YAANI YATIMA)**

5. a. Jina la Mlezi.....................................................................................................................

b. Uhusiano kati ya Mlezi na Mwanafunzi......................................................................

c. Kazi ya Mlezi............................................ Simu na......................................................

d. Anuani ya Mlezi............................................................................................................

6. Shule atokayo mwanafunzi...........................................................................................

7. Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi? ..........................................................

8. Maelezo ya mwanafunzi ....................................................................................................
.......................................... ..........................................................................................

9. Ujuzi/stadi nyingine.........................................................................................................

Sahihi ya Mwanafunzi ............................................................ Tarehe................../.........../..................

KIAMBATANISHO B: FOMU YA KUMUANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI

OFISI YA RAIS UTUMISHI, TAMISEMI NA UTAWALA BORA

SHULE YA SEKONDARI MABWEREBWERE

Mimi ........................................................................................................... msichana/mvulana ninakubali kuingia kidato cha ................. katika shule ya sekondari **MABWEREBWERE**
Kama mwanafunzi wa kutwa tarehe............../................/......................
Nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria, kanuni na taratibu zote za shule pamoja na maelekezo yote nitakayopewa na walimu au viongozi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea, nitalazimika kulipa uharibifu wowote uwe ni wa majengo, vitabu au kitu chochote nitakavyoharibu/nitakachopoteza nikiwa shuleni ama nje ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi......................................................... Tarehe.........../.............../..............

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:
Mimi.......................................................................................................................... ninakubali mtoto wangu ............................................................................... asome katika shule ya sekondari **MABWEREBWERE** kuanzia tarehe.............../.............../.................... Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa na atakayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ilivyotajwa katika barua hii na kadri itakavyoelekezwa na uongozi wa shule.
Ninakuhakikishia kwamba nitamhimiza mtoto wangu kutii sheria za shule, kuwa na nidhamu, adabu na heshima; pamoja na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.

Nakirii kuwa mtoto wangu amekubali kuingia katika/kujiunga na shule ya sekondari MABWEREBWERE kama mwanafunzi wa kutwa. Hivyo muda wa mwanafunzi kuwa shuleni ni saa moja kamili asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana. Aidha nitawajibika kwa malezi ya ziada kwa muda ambao si wa masomo, siku za mapumziko a wakati wa likizo.

Anuani yangu ya kudumu ni:
.......................................................................................................................................................
Sahihi.........................................................................tarehe................../............./..................
SIMU..........................................................................

APENDEX C: MEDICAL EXAMINATION FORM

MABWEREBWERE SECONDARY SCHOOL

P.O BOX 50

KILOSA

Mob……………………………………………….

Date…………/…………/…………………

PART A:

Mr./miss……………………………………………………………………………………………………………

Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for full time student in this school. The examination should include the following:

1. Hemoglobin……………………………………………………………………………………………………
2. P.V bleeding……………………………………………………………………………………………………
3. Sight……………………………………………………………………………………………………………
4. Blood pressure…………………………………………………………………………………………………
5. Urine for sugar…………………………………………………………………………………………………
6. Stool for routine examination……………………………………………………………………………
7. Pregnancy test…………………………………………………………………………………………………
8. Skin diseases……………………………………………………………………………………………………
9. Leprosy…………………………………………………………………………………………………………
10. Any deformity…………………………………………………………………………………………………
11. Epilepsy…………………………………………………………………………………………………………
12. Pulmonary tuberculosis……………………………………………………………………………………
13. Neurosis…………………………………………………………………………………………………………
14. Venereal diseases……………………………………………………………………………………………
15. Other serious diseases……………………………………………………………………………………

**PART B:**

**(To be completed by Government Medical Officer)**

1. I have examined the above named student and consider that he/she is physically fit/unfit for a full time schooling.
2. Other Comments:

   ……………………………………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………………………………………
3. Date ……………/……………/……………. signature………………………………………………………

   Station…………………………………………………. Designation………………………………………………

   Official stamps…………………………………………………